

WACHUNGAJI WAZAWA NCHINI TANZANIA

Re-arranged and translated by Pastor Stephen Letta

Raphael Chacha Megera, (1922–2009)

Raphael Chacha Megera alikuwa mwalimu, mchungaji, na msimamizi nchini Tanzania.

Maisha ya Awali, Elimu, na Ndoa

Raphael Chacha Megera alizaliwa mwaka 1922 katika kijiji cha Nyarero, Tarime, Tanzania, huko Megera. Twebe (c.1890-1962) na Businge Musintani (1900-1950). Raphael alikuwa wa pili kuzaliwa kati ya ndugu saba. Alitumia maisha yake ya awali huko Nyarero na vijiji vya jirani vya Nyamongo, Mogabiri, na Utimbaru. Alikubali imani ya Waadventista alipokuwa akisoma shule ya msingi ya Kibumaye kuanzia 1936 hadi 1939. Kuanzia 1940 hadi 1948, alisoma shule ya Ikizu kwa elimu ya kati na sekondari. Alihudhuria Shule ya Mafunzo ya Ualimu ya Ikizu mwaka wa 1949. Mwaka 1953 na 1954 alihudhuria Seminari ya Waadventista ya Bugema kwa mafunzo ya uchungaji. Mnamo 1961 na 1962, alihudhuria Chuo Kikuu cha Solusi.

Megera alimuoa Rahabu Nyakorema Thomas mwaka 1946 kwenye Kanisa la SDA Nyariso. Rahab alizaliwa mwaka 1932. Hao wawili walizaa watoto saba: Gati, Rhobi, Wegesa, Otaigo, Twebe, Mbota, na Mataro.

Uchungaji:

Kuanzia 1945 hadi 1955, Megera alihudumu katika shule za kanisa la Waadventista kama mwalimu. Mwaka 1956 alijiunga na huduma ya kichungaji na akahudumu kama mchungaji wa mstari wa mbele hadi 1960. Kisha, huduma yake ikageukia katika kusimamia fedha za kanisa: akawa mweka hazina wa Shule ya Ufundi ya Ikizu (1963-1964), mhasibu wa Tanzania Union Mission (1965-1967), katibu-mhazini wa East-Lake Tanzania Field), Mhasibu wa Union Misheni ya Tanzania (1969-1971), mweka hazina msaidizi na mkaguzi wa Union Misheni ya Tanzania (1972-1976), mweka hazina wa Union Misheni ya Tanzania (1977-1984), mkaguzi wa Divisheni ya Afrika Mashariki (1985-1989), na mweka hazina na mkaguzi msaidizi katika Union ya Afrika Mashariki, Kenya-1990).

Kustaafu

Raphael Megera alistaafu utumishi mwaka 1993 na aliishi Arusha mjini hadi kifo chake Machi 15, 2009.